# Ripoti iliyoandikwa kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi and Sekondari

## Utangulizi

Kama mzazi/mlezi/mwangalizi utapokea ripoti mbili zilizoandikwa kila mwaka. Ripoti hizi zitasaidia kuelewa jinsi mtoto wako anaendelea na jinsi shule inavyosaidia maendeleo ya mtoto wako.

Walimu wanapanga, kufundisha, kutathmini na kutoa ripoti ya kujifunza ya wanafunzi kwa kutumia Australian Curriculum. Mtaala wa Australia hutunga viwango vya juu kwa ajili ya vijana wa Australia wanavyopaswa kufundishwa na nini wanapaswa kujua na kuweza kufanya wakati wanaendelea na masomo ya shule.

Kila sehemu ya masomo ina viwango vya mafanikio. Viwango hivi huelezea kwa lugha nyepesi vitu ambavyo wanafunzi wanapaswa kujua kwa kawaida, kuelewa na kuwa na uwezo wa kufanya, kwa kila mwisho wa ngazi ya mwaka.

Unahimizwa kusoma viwango kwa kila eneo la somo hilo na ngazi ya mwaka, na wakati wanafunzi wanatarajiwa kufikia hayo, kwenye tovuti ya Mitaala ya Australia:: www.australiancurriculum.edu.au. Tovuti hiyo pia inajumuisha mifano na manufaa ya kazi ya wanafunzi katika ngazi mbalimbali za mafanikio.

## Ni mahitaji yapi kwa ajili ya ripoti ya mwanafunzi?

Taarifa zilizoandikwa ni njia mojawapo tu ambayo shule zinawasiliana na wewe kuhusu jinsi mtoto wako anavyoendelea shuleni.

Shule zote katika Australia ya Kusini huwapa wazazi na walezi ripoti mbili zilizoandikwa kila mwaka ambazo:

- hutoa taarifa ya masomo yote yaliyosomwa na mtoto wao
- yanalenga katika viwango 5 vya mafanikio
- hutumia lugha nyepesi
- kutambua maeneo ya nguvu na maeneo yanayohitaji maendeleo zaidi.

Ripoti za wanafunzi wa mwaka wa 1-10 hutolewa katika kipimo cha A-E cha mafanikio, ikiungwa mkono na maelezo ya kitu gani inamaanisha maana kuhusiana na maendeleo yao dhidi ya mafanikio ya kiwango.

Ripoti kwa wanafunzi wa Mapokezi hutumia maelezo ya maneno kuhusu maendeleo ya wanafunzi 'katika mwaka ikilinganishwa na kiwango cha mafanikio katika Mapokezi.

## Je walimu wanapanga namna gani kiwango?

Walimu hutumia aina ya mikakati mbalimbali ya tathmini na zana ili kukusanya ushahidi wa mafanikio ya mwanafunzi kwa kuzingatia viwango vya mafanikio katika Mitaala ya Australia. Kulingana na ushahidi, walimu hufanya uamuzi kwa kuzingatia usawa ili kuamua ni daraja lipi linalingana na kiwango cha mafanikio ya mwanafunzi. Walimu hawatarajiwi kutenga idadi ya seti ya kila daraja ndani ya darasa lao.

## Aina gani nyingine ya taarifa inayotolewa na shule?

Shule huwasiliana na wewe kuhusu kujifunza kwa mtoto wako katika njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na mahojiano ya mzazi na mwalimu. Unaweza kuomba mahojiano wakati mwingine kwa kuwasiliana na shule ili kuomba mda mzuri kukutana na mwalimu wa mtoto wako.

# Daraja la A-E lina maana gani?

Daraja au maneno ya ulinganisho hutumiwa na walimu wa ripoti ya mafanikio ya wanafunzi 'dhidi ya viwango vya mafanikio vya mitaala ya Australia. Daraja huelezea aina mbalimbali ya mafanikio kutoka ndogo kwenda kubwa.

Jedwari linalofuata huelezea kila daraja katika maneno.

| | *Kulingana na viwango vya mafanikio, mtoto wako …* |
|---|---|
| *A* | *ni kuonyesha mafanikio **bora zaidi** ya mambo yanayotarajiwa katika ngazi hii ya mwaka.* |
| *B* | *ni kuonyesha mafanikio **mazuri** ya mambo yanayotarajiwa katika ngazi hii ya mwaka.* |
| *C* | *ni kuonyesha mafanikio ya **wastani** ya mambo yanayotarajiwa katika ngazi hii ya mwaka.* |
| *D* | *ni kuonyesha mafanikio **kidogo** ya mambo yanayotarajiwa katika ngazi hii ya mwaka.* |
| *E* | *ni kuonyesha mafanikio ya **chini** ya mambo yanayotarajiwa katika ngazi hii ya mwaka.* |

- Daraja "A" inaonyesha kuwa mwanafunzi ameonyesha elimu ya uhakika na uelewa wa mada na anaweza kutumia mafunzo katika hali tofauti.
- Kwa kawaida daraja 'C' ina maana mwanafunzi anafikia mambo yanayotarajiwa wakati huo katika mafunzo yao. Haya ni mafanikio makubwa kwa sababu ya matarajio ya juu yaliyoundwa katika viwango vya mafanikio.
- Daraja 'E' ina maana mwanafunzi yuko anaanza tu kufanya kazi katika kufikia kiwango.

Daraja A-E na maoni yanayoandamana ni sehemu moja ya kutoa taarifa kwa wazazi /walezi/ wasimamizi. Ripoti inaweza pia kutoa taarifa kuhusu:

- uwezo wa mwanafunzi na maeneo kwa ajili ya maendeleo
- mikakati ya kusaidia maendeleo yao
- mtazamo na dhamira ya kujifunza
- taarifa kuhusu maendeleo yao ya kijamii
- kuhusika katika mipango na shughuli za shule
- mahudhurio

Maamuzi juu ya muundo na maudhui ya ripoti za shule hutolewa na shule kwa kushauriana na jumuiya yao.

# Je ripoti zote za wanafunzi zinajumuisha daraja A-E?

Maendeleo na mafanikio ya baadhi ya wanafunzi yatatolewa taarifa juu ya mafanikio ya kiwango ambacho kinalingana na kiwango chao cha sasa cha mafanikio. Hii inaweza kutokea katika baadhi ya maeneo ya kujifunza. Mda mwingine, mafanikio yao yanaweza kulinganishwa na malengo ya mpango wao binafsi wa kujifunza. Shule zinatarajiwa kujadili mpango mwanafunzi wa kujifunza na mipangilio sahihi ya kutoa taarifa kwa baadhi ya wanafunzi na wazazi /walezi/walezi pamoja na mwanafunzi kama inafaa, na wataalamu wengine muhimu.

Hii inaweza kutokea kwa baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu na wanafunzi wapya waliowasili karibuni wanaostahili katika shule tawala. Wanafunzi ambao wameacha Mpango wa Lugha ya Kiingereza / Mpango wa Wahamiaji Wapya (IELP / NAP) wanaweza wasipewe daraja A-E hadi mihura sita baada ya kuondoka katika mpango husika. Wanafunzi katika IELP / NAP hupokea ripoti inayoeleza mafanikio yao badala ya daraja A-E.